TANGAZO LA SERIKALI NA. 643 la tarehe 26/7/024

SHERIA YA PETROLI,
(SURA YA 392)

## KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 246)*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA USULUHISHI WA MIGOGORO ITOKANAYO NA SHUGHULI ZA MKONDO WA JUU WA PETROLI ZA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 632 la 2023

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Usuluhishi wa Migogoro Itokanayo na Shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli za Mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Usuluhishi wa Migogoro Itokanayo na Shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli za Mwaka 2023, ambazo hapa zimerejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 18

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 18 kwa kufuta rejea ya "kanuni ya 18" iliyo katika kanuni ndogo ya (1) na badala yake kuweka "rejea ya kanuni ya 17".

Marekebisho ya kanuni ya 23

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 23-
(a) kwa kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (1) kanuni ndogo ifuatayo:

"(2) Ukomo wa muda wa usikilizwaji wa mgogoro utakua kama ifuatavyo:

(a) ukomo wa muda wa usikilizwaji wa kwanza utakuwa kwa mgogoro ambao Kamati inaona ni mgogoro wa haraka ambao kwa maslahi ya haki unatakiwa kuamuliwa ndani ya kipindi kisichozidi miezi minne tangu tarehe ya kuweka ukomo wa

muda wa usikilizwaji; na

(b) ukomo wa muda wa usikilizwaji wa pili utakuwa kwa mgogoro ambao Kamati inaona ni mgumu, ambao kwa maslahi ya haki unatakiwa kuamuliwa ndani ya kipindi kisichozidi miezi kumi tangu tarehe ya kuweka ukomo wa muda wa usikilizwaji.”;

(b) kwa kufuta rejea ya kanuni ndogo ya (3) iliyo katika kanuni ndogo ya (4) na badala yake kuweka rejea ya kanuni ndogo ya (4); na

(c) kwa kubadili mpangilio wa kanuni ya (2), (3), (4) na (5) kuwa kanuni ya (3), (4), (5) na (6) mtawalia.

Marekebisho ya kanuni ya 45

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 45 kwa kufuta maneno “atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu” na badala yake kuweka maneno “anatenda kosa na akikutwa na hatia atawajibika kulipa faini iliyoanishwa kwenye Sheria”.

Dodoma, ………………….., 2024

CHARLES SANGWENI
*Mkurugenzi Mkuu*